JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

CHUO CHA UALIMU KOROGWE

S. L. P. 533

KOROGWE.

Simu 027 2640540

027 2640847

Fax: 027 2640999

Email: korogwettc@gmail.com

19 July, 2013

Kumb. Na.KTC/Reg/Vol.1/121/……..

Ndugu …….

S.L.P. ……..

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA CHETI DARAJA A / STASHAHADA MWAKA WA MASOMO 2013/2014

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi** imekuchagua kujiunga na mafunzo ya ualimu ngazi ya Stashahada katika chuo hiki kwa mwaka wa masomo **2013/2014**.Masomo utakayosomea ni …… **Hongera sana.**

Chuo cha Ualimu Korogwe kipo katika mkoa wa **Tanga**, wilaya ya **Korogwe**,kilometa moja **(km 1)** kutoka stendi kuu ya mabasi Korogwe mjini. Ukishuka basi fuata barabara iendayo Hospitali ya Wilaya ya Korogwe **(MAGUNGA HOSPITAL)** upande wa **Kaskazini.** Ukipenda unaweza kukodi **bajaji** ili ufike chuoni haraka. Dira ya chuo chetu ni **"Kutoa Elimu Bora"** na Moto wa chuo ni **"Mwalimu kwa Mfano".**

Ili uweze kusajiliwa kwa mafunzo haya unapaswa kufika chuoni na mahitaji yafuatayo:

(A) Nyaraka za Kiofisi

1. Barua ya maelekezo ya kujiunga na chuo hiki (**Joining instructions letter**) uliyotumiwa kutoka hapa chuoni
2. Vyeti vyote halisi vya kitaaluma **(academic certificates)** vya kidato cha nne na cha sita na vyeti vya marudio ya mitihani na vivuli vyake;

korogwe tc 2013

3. Vyeti vya kumaliza kidato cha nne na sita na vivuli vyake **(Leaving Certificates)**;
4. Cheti halisi cha **Ualimu Daraja la IIIA** na kivuli chake kama wewe ni mwalimu;
5. Cheti cha kuzaliwa na kivuli chake;
6. Barua ya ruhusa kutoka kwa mwajiri wako kama wewe ni mwajiriwa;
7. Picha mbili za ***passport size*** za rangi zenye ubora **(lightblue background)**
8. Form ya kupimwa afya iliyojazwa na kusainiwa na daktari wa hospitali ya serikali. Fomu hiyo imeambatanishwa na barua hii.

(B) Ada na Michango

1. Ada ya chuo **TSh.200,000**/= kwa mwaka. Unaweza kulipa **TSh.100,000/=**kwa muhula; Ada hii ilipwe kupitia akaunti ya Chuo ilipo katika **Benki ya NMB** ambayo ni ***Korogwe TTC Revenue Account No. 4151000014***
2. Mazoezi ya kufundisha (BTP) **Tsh 13,000/=**
3. Matibabu **TSh.10,000/=** kwa mwaka;
4. Ujenzi wa maktaba **TSh.10,000/=** kwa mwaka;
5. Usajili **TSh.5,000/=** kwa mwaka wa kwanza tu
6. Serikali ya wanachuo **TSh.5,000/=** kwa mwaka;
7. Taaluma Kanda **TSh.20,000/=** (kwa mtihani wa kuingia mwaka wa pili)
8. Kukodisha Godoro **TSh. 10,000/=** kwa mwaka;
9. Mahafali **TSh.5,000/=** kwa mwaka;
10. Kitambulisho **Tsh.5,000/=** unapoanza mafunzo mwaka wa kwanza.
11. Michezo TSh. **10,000/=** kwa mwaka;
12. Ulinzi **Tsh.3,000/=** kwa mwaka;
13. Mafunzo ya ICT/TEHAMA **TSh.10,000/=** kwa mwaka;
14. Ukarabati **TSh. 10,000/=** kwa mwaka;

Michango mingine ya chuo kuanzia namba **2** hadi **14** ilipwe katika akaunti ya chuo iliyopo **NMB** ambayo ni ***Principal Korogwe T.C Account No.4151100012***

korogwe tc 2013

(C) Sare ya Chuo

Wanachuo wote wanapaswa kuwa katika sare ya Chuo wakati wote wa vipindi vya masomo na wanapotoka nje ya chuo.

(i) Sare kwa Wanachuo wa Kike

1. Sketi **mbili nyeusi** zisizo za kubana na ziwe ndefu kiasi cha **kuvuka magoti**. Kila moja iwe na ***rinda boksi*** moja mbele;
2. Mashati mawili ya mikono mirefu rangi ya bluu **bahari (light blue)** na koti jeusi (*ukipenda*);
3. Jozi mbili za **viatu vyeusi** vya kuchomeka visivyo na visigino virefu na jozi mbili za **soksi nyeupe**;
4. Tai ndogo ya rangi **nyeusi (butterfly tie);**
5. Hijab kwa wanachuo wa Kiislam; nusu **kanzu mbili** za rangi ya **bluu bahari,** vitambaa viwili vya bluu bahari na **suruali mbili,** za kike za **rangi nyeusi** au **siketi mbili ndefu** nyeusi. Nusu kanzu na suruali zisiwe za kubana.
6. Mavazi ya michezo

(ii) Sare ya Wanachuo wa Kiume

1. Suruali mbili za rangi **nyeusi**. *Jeans* haziruhusiwi;
2. Mashati mawili ya mikono mirefu ya rangi ya **bluu bahari (light blue)** na **koti jeusi** (*ukipenda*);
3. Jozi mbili za **viatu vyeusi** vya kuchomeka na visivyo na visigino virefu na jozi mbili za soksi nyeusi;
4. Tai ndefu ya rangi nyeusi;
5. Mavazi ya michezo

(D) Vifaa Vingine

1. Shuka mbili za **rangi ya pinki** kwa wasichana na **bluu bahari (light blue)** kwa wavulana;
2. Bunda moja la karatasi za kurudufisha **(Maestro the standard paper for black/white applications for Laser, Inkjet Printers and copiers)**

NB: mifano ya mishono ya sare za chuo zinazohitajika zipo ukurasa wa 5

Wasilisha katika ofisi ya Usajili na ofisi ya Uhasibu ***bank pay -in-slips*** za malipo haya ili uweze kusajiliwa na kupata stakabadhi za Chuo.

korogwe tc 2013

Kabla hujaanza safari ya kuja Chuoni hakikisha umezisoma na kuzielewa **Nguzo Adili za Chuo** na **umekubali kuzifuata**. Utovu wowote wa nidhamu hautavumiliwa. Halikadhalika, hakikisha kuwa umekamilisha mahitaji yote uliyoagizwa kuja nayo.

Kwa niaba ya Jumuiya ya Chuo napenda kukukaribisha Chuoni na kukutakia mafanikio mema ya kielimu.

.....

LYANA J.M.

MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU, KOROGWE

Nakala kwa: Mkurugenzi,

Idara ya Elimu ya Ualimu,

S.L.P. 9121

Dar es Salaam.

korogwe tc 2013

SKETI



SURUALI



korogwe tc 2015